Zana ya Kutathmini Eneo la Kuchimba Madini

Jina la eneo la mgodi:	
Jina la kampuni:	
Eneo:	
Tarehe:	

01 Ajira kwa Wanaoishi katika Eneo husika

	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Hufichua hadharani idadi ya **watu wanaotoka kwenye jamii husika** ambao hufanya kazi kama **wafanyakazi**?	☐	☐
b.	Hufichua hadharani idadi ya **watu wanaotoka kwenye jamii husika** ambao hufanya kazi kwa **wakandarasi**?	☐	☐
c.	Hufichua hadharani idadi ya **wanawake wanaotoka kwenye jamii husika** ambao wameajiriwa kama wafanyakazi na ambao hufanya kazi kwa wakandarasi?	☐	☐
d.	Hufichua hadharani idadi ya watu wanaotoka kwenye jamii husika ambao wanafanya kazi kama wafanyakazi na ambao wanawafanyia kazi wakandarasi **ambao wamepandishwa cheo na kupewa nafasi za juu**?	☐	☐

02 Kupata Bidhaa na Huduma za Eneo

	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Hifichua hadharani **kiasi cha pesa** inachotumia kupata bidhaa na huduma kutoka katika eneo husika?	☐	☐
b.	Hufichua hadharani **aina za bidhaa na huduma** inazonunua kutoka katika eneo husika?	☐	☐
c.	**Huhusisha jamii husika katika kubuni** mipango yake ya kupata bidhaa na huduma za eneo husika?	☐	☐
d.	**Huhusisha pakubwa wanawake kutoka katika jamii husika katika kubuni** mipango yake ya kupata bidhaa na huduma za eneo husika?	☐	☐

03 Ubora wa Hewa

	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Hufichua hadharani mara kwa mara, **data ya ubora wa hewa kwa kila sehemu ya ufuatiliaji**?	☐	☐
b.	**Huangazia** mahali na wakati ambapo ubora wa hewa hupungua chini ya vikomo vya usalama?	☐	☐
c.	**Huhusisha jamii husika katika kufanya maamuzi** ya kudhibiti ubora wa hewa?	☐	☐
d.	**Huhusisha pakubwa wanawake kutoka jamii husika katika kufanya maamuzi** ya kudhibiti ubora wa hewa?	☐	☐

04 Ubora wa Maji

	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Hufichua hadharani mara kwa mara, **data ya ubora wa maji kwa kila sehemu ya ufuatiliaji?**	☐	☐
b.	**Huangazia** mahali na wakati ambapo ubora wa maji hupungua chini ya vikomo vya usalama?	☐	☐
c.	**Huhusisha jamii husika katika kufanya maamuzi** ya kudhibiti ubora wa maji?	☐	☐
d.	**Huhusisha pakubwa wanawake kutoka jamii husika katika kufanya maamuzi** ya kudhibiti ubora wa maji?	☐	☐

05 Wingi wa Maji

	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Hufichua mara kwa mara, **kiasi cha maji ambacho inatumia** kutoka kwenye mazingira?	☐	☐
b.	**Hujadiliana na jamii husika kuhusu jinsi ya kudhibiti uwezo wa kufikia** rasilimali za maji zinazoshirikiwa?	☐	☐
c.	**Huhusisha pakubwa wanawake kutoka jamii husika katika kujadiliana jinsi ya kudhibiti uwezo wa kufikia** rasilimali za maji zinazoshirikiwa?	☐	☐
d.	Huhusisha jamii husika katika **maamuzi yanayofanywa ili kudhibiti matumizi yake ya maji?**	☐	☐

06	**Kurejesha Hali ya Kawaida ya Eneo na Shughuli za Baada ya Kufunga Eneo la Kuchimba Madini**		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Huhakikisha kuwa jamii husika zimefahamishwa kuhusu **wakati shughuli za eneo la kuchimba madini zitakaposimamishwa au eneo la kuchimba madini litakapofungwa?**	☐	☐
b.	**Huhusisha jamii husika katika kubuni** mipango yake ya shughuli za baada ya kufungwa kwa eneo la kuchimba madini na kurejesha hali ya kawaida ya eneo?	☐	☐
c.	Huhakikisha kuwa **jamii husika zimekubaliana na** mipango ya shughuli za baada ya kufungwa kwa eneo la kuchimba madini na kurejesha hali ya kawaida ya eneo kwa jamii?	☐	☐
d.	**Huhusisha pakubwa wanawake kutoka jamii husika katika kubuni na kuidhinishwa** kwa mipango yake ya shughuli za baada ya kufungwa kwa eneo la kuchimba madini na kurejesha hali ya kawaida ya eneo?	☐	☐

07	**Udhibiti wa Mabaki**		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Hufichua hadharani **eneo kamili** la maeneo yake yote ya kuhifadhi mabaki?	☐	☐
b.	Huhakikisha kuwa maeneo yake yote ya kuhifadhi mabaki **yametiwa sahihi kwa njia zinazoweza kueleweka kwa urahisi na kufanywa kuwa salama** kwa watu na wanyama?	☐	☐
c.	Hufichua hadharani **eneo kamili la jiografia ambalo linaweza kuathiriwa na hitilafu za mabwawa yake ya mabaki?**	☐	☐
d.	**Hujaribu mara kwa mara ving’ora na mifumo mingine ya onyo** ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi na jamii husika zinataarifiwa iwapo kutatokea ajali zozote za mabwawa ya mabaki?	☐	☐

08	**Usalama wa Jamii**		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Hufichua hadharani **idadi na hali za vifo** ambavyo hutokea katika eneo lake la kuchimba madini lililoidhinishwa?	☐	☐
b.	Huhakikisha kuwa jamii husika **zimefahamishwa kuhusu jambo la kufanya** iwapo dharura inayohusiana na uchimbaji madini itatokea?	☐	☐
c.	**Huhusisha jamii husika katika kujaribu** mipango hii ya kukabiliana na dharura?	☐	☐
d.	**Huhusisha pakubwa wanawake kutoka jamii husika katika kujaribu** mipango hii ya kukabiliana na dharura?	☐	☐

09	**Malalamiko na Manung'uniko ya Jamii**		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ina **mbinu ya kushughulikia manung'uniko kwa jamii husika** na watu kuwasilisha malalamiko na manung'uniko?	☐	☐
b.	Huhakkikisha kuwa wafanyakazi wa kiume na wa kike wanapatikana ili kupokea na kushughulikia manung'uniko ya jamii ili **wanawake kutoka jamii husika waweze kuzungumza na mtu wa jinsia sawa na yao?**	☐	☐
c.	Hufichua hadharani **idadi na aina ya malalamiko manung'uniko** yanayowasilishwa na watu na jamii husika?	☐	☐
d.	**Hujadiliana na jamii husika kuhusu mbinu ambayo inachukua ili** kuepuka kutokea tena kwa malalamiko manung'uniko sawa na hayo?	☐	☐

10	**Usalama na Afya ya Wafanyakazi**		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Hutoa **vifaa vya usalama vinavyofaa** kwa wafanyakazi wake wote na watu wanaofanyia kazi wakandarasi, bila malipo?	☐	☐
b.	Hutoa **vifaa vya usafi na ubadilishaji vinavyofaa** kwa wafanyakazi wake wote na watu ambao hufanya kazi kwa wakandarasi?	☐	☐
c.	Huhakikisha kuwa **wafanyakazi wa kike** wote wana uwezo wa kufikia vifaa vya usafi na ubadilishaji vinavyofaa ambavyo ni salama na **vilivyotengwa na vile vinavyotumiwa na wafanyakazi wa kiume?**	☐	☐
d.	Hufichua hadharani **saa za wastani za kila mfanyakazi kufanya kazi na kwa siku?**	☐	☐

11 Wafanyakazi wa Kike

	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Huchukua hatua za **kuzuia unyanyasaji wa wafanyakazi wa kike?**	☐	☐
b.	Huchukua hatua za **kuzuia vurugu za kijinsia dhidi ya wafanyakazi wa kike?**	☐	☐
c.	Huhakikisha utoaji wa **nguo za kufanyia kazi na vifaa vya ulinzi wa binafsi ambavyo vinafaa** kwa miili ya wafanyakazi wa kike na wanawake wanaofanya kazi kwawakandarasi?	☐	☐
d.	Hutoa **mafunzo ya uhamasishaji wa jinsia** kwa wafanyakazi wake wote na watu wanaofanyia kazi wakandarasi?	☐	☐

12 Majeraha na Vifo Vinavyotokea Mahali pa Kazi

	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Hufichua hadharani **idadi na hali za majeraha na vifo vya wafanyakazi wake** ambavyo hutokea mahali pa kazi?	☐	☐
b.	Hufichua hadharani **idadi na hali za majeraha na vifo vya watu wanaofanya kazi kwa wakandarasi** ambavyo hutokea mahali pa kazi?	☐	☐
c.	Ina **kamati ya pamoja ya afya na usalama wa kazini** iliyotungwa na wawakilishi wa wafanyakazi na waajiri ili kutathmini hatari na kuchunguza matukio?	☐	☐
d.	Huhakikisha kuwa **wafanyakazi wa kike wamewakilishwa** kwenye kamati ya pamoja ya afya na usalama wa kikazi?	☐	☐

13 Mafunzo ya Wafanyakazi

	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Huhakikisha kuwa watu na wafanyakazi wote ambao hufanya kazi kwa wakandarasi wanapokea **maagizo ambayo yanahitajika** ili kufanya kazi zao kwa usalama na bila kupata majeraha?	☐	☐
b.	Hutoa mafunzo kwa wafanyakazi bila malipo, **ili kukuza ujuzi wao wa kiufundi?**	☐	☐
c.	Huhakikisha kuwa **wafanyakazi wa kike wanaweza kufikia mipango yote ya mafunzo** na fursa za kujifunza?	☐	☐
d.	**Huhusisha watu na wafanyakazi wote ambao hufanya kazi kwa wakandarasi katika kujaribu** mipango yake ya kushughulikia dharura?	☐	☐

14	**Mshahara wa Kuwezesha Kuishi Maisha Mazuri**		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	**Hutathmini kiwango cha mshahara** ambao unahitajika na wafanyakazi na familia zao ili kumudu kuishi maisha mazuri?	☐	☐
b.	Huhakikisha kuwa **mishahara** ya wafanyakazi wake wote inafikia au inazidi kiwango hiki cha mshahara wa kuwezesha kuishi maisha mazuri?	☐	☐
c.	Huhakkikisha kuwa mishahara ya watu wote ambao hufanya kazi kwa **wakandarasi** pia inafikia au inazidi kiwango hiki cha mshahara wa kuwezesha kuishi maisha mazuri?	☐	☐
d.	Hufichua hadharani **kiwango cha mshahara wa chini zaidi kwa wafanyakazi wa kiume na wa kike** kwa kila kiwango cha kazi?	☐	☐

15	**Malalamiko na Manung'uniko ya Wafanyakazi**		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ina **mbinu ya kushughulikia manung'uniko ya wafanyakazi wake na watu wanaofanya kazi kwa wakandarasi** ya kuwasilisha malalamiko/manung'uniko?	☐	☐
b.	Huhakikisha kuwa wafanyakazi wa kiume na wa kike wanapatikana ili kupokea na kushughulikia manung'uniko ya wafanyakazi ili **wafanyakazi wa kike waweze kuzungumza na mtu wa jinsia sawa na yao?**	☐	☐
c.	Hufichua hadharani **idadi na aina ya malalamiko/manung'uniko** yaliyowasilishwa na wafanyakazi wake na watu wanaofanya kazi kwa wakandarasi?	☐	☐
d.	**Hujadiliana na wafanyakazi, wafanyakazi wa wakandarasi na wawakilishi wao kuhusu hatua ambazo inachukua** ili kuepuka kutokea tena kwa malalamiko/manung'uniko sawa na hayo?	☐	☐

Maoni:

Kuhusu

01 Ajira kwa Wanaoishi katika Eneo husika

Kampuni ambayo hufichua idadi ya watu wanaoishi katika eneo ambao hufanyia kazi katika eneo lake la kuchimba madini inaweza kuonyesha kujitolea kwake katika kuwekeza kwenye maendeleo ya kiuchumi ya jamii za eneo husika hilo. Hatua ya kufichua data mahususi kuhusu wafanyakazi wa kike huisaidia kampuni kuonyesha kuwa mchakato wao wa kuajiri wafanyakazi na desturi za mahali pa kazi hazibagui dhidi ya wanawake. Kampuni inaweza kutoa picha kamili zaidi ya hali ya ajira kwa kuonyesha idadi ya watu wanaoishi katika eneo husika ambao wanafanyia kazi wakandarasi wake.

02 Kupata Bidhaa na Huduma za Eneo

Kampuni ambayo hununua bidhaa na huduma za eneo husika inaweza kuchangia ukuaji wa biashara na ukuaji wa uchumi katika eneo husika. Kampuni inapotoa maelezo kuhusu kupata bidhaa na huduma za eneo, inasaidia biashara za eneo kutambua fursa za kuwa wasambazaji wa bidhaa na huduma kwa eneo la kuchimba madini na inaonyesha pia jinsi inavyohimiza biashara za eneo kuwa wasambazaji wa bidhaa na huduma.

03 Ubora wa Hewa

Uchafuzi wa hewa ni wasiwasi mkubwa kwa jamii nyingi zinazoathiriwa na kuwepo kwa eneo la kuchimba madini, kwa sababu uchafuzi wa hewa unaweza kuathiri afya zao, mimea yao ya chakula, mifugo yao na wakati mwingine mapato yao. Kampuni inapofichua hadharani data kuhusu ubora wa hewa karibu na eneo la kuchimba madini na kujadiliana na jamii kuhusu jinsi inavyodhibiti ubora wa hewa, inaweza kujenga imani na kupunguza hofu inayohusiana na vumbi na uchafuzi wa hewa.

04 Ubora wa Maji

Kampuni inaweza kufanya maelezo yake ya umma kuhusu ubora wa maji yawe ya manufaa zaidi kwa jamii husika kwa kufichua mara kwa mara data ya ubora wa maji katika kila sehemu ambako inakusanya data kama hiyo. Kampuni pia inaweza kujenga imani kwa kubainisha mahali na wakati ambapo ubora wa maji ulipungua chini ya vikomo vya usalama na kwa kujadiliana na jamii husika juhudi ambazo inachukua ili kudhibiti ubora wa maji.

05 Wingi wa Maji

Uwezo wa kufikia maji ni chanzo cha kawaida cha migogoro kati ya kampuni za kuchimba madini na jamii husika, hasa katika maeneo yaliyo na uchache wa maji. Kampuni inaweza kuonyesha heshima yake kwa jamii husika kwa kufichua kiasi cha maji inachotumia kutoka kwa vyanzo vya eneo husika na kwa kujadiliana na jamii husika jinsi matumizi yake ya maji yanavyozingatia mahitaji ya maji ya watu wanaoishi katika eneo husika.

06 Kurejesha Hali ya Kawaida ya Eneo na Shughuli za Baada ya Kufunga Eneo la Kuchimba Madini

Ili kampuni iweze kuacha athari nzuri kwenye eneo lililo karibu na eneo lake la kuchimba madini, inahitaji kuhakikisha kuwa jamii husika zitakuwa na mapato ya kudumu eneo la kuchimba madini litakapofungwa. Hii inajumuisha kuhakikisha kuwa watu wanaoishi katika eneo husika wataweza kutegemea rasilimali asili zenye ubora wa juu (ardhi, maji nk.) na fursa za kibiashara. Kampuni pia itahitaji kujadili na kuidhinisha mpango wa kufungwa kwa eneo la kuchimba madini na jamii husika ili kuzingatia jinsi watu wanaoishi katika eneo husika wanavyotaka eneo lionekane baada ya eneo la kuchimba madini kufungwa.

07 Udhibiti wa Mabaki

Mabwawa ya mabaki yanaweza kuwa hatari zaidi kwa watu, mifugo na mazingira. Iwapo mabwawa ya mabaki yatavunja kingo zake, yanaweza kuachilia kiasi kikubwa cha uchafu ambao unaweza kusababisha vifo, kufunika mito, kuzika maboma, kuharibu mapato na kuathiri vibaya sana mazingira na jamii za eneo husika kwa miaka mingi ijayo. Kampuni inaweza kuonyesha kuwa inachukulia suala hili kwa uzito zaidi kwa kufichua maelezo yanayoweza kutekelezwa kwenye mabwawa yake ya mabaki, kwa kuhakikisha kuwa mabwawa haya yametiwa sahihi kwa njia dhahiri na kufanywa kuwa salama ili kuzuia majeraha ya ajali au vifo vya watu na wanyama na kwa kujaribu mara kwa mara mifumo ya onyo.

08 Usalama wa Jamii

Kwa kawaida uchimbaji madini ni hatari kwa jamii za eneo husika, kwa sababu ajali na migogoro inaweza kusababisha vifo na majeraha. Kampuni inaweza kuheshimu jamii za eneo husika na kusaidia kudumisha usalama wao kwa kufichua hadharani idadi na hali za vifo vyovyote ambavyo vinatokea. Ingawaje ni vigumu kutoa hakikisho kuwa hali za dharura zinazohusiana na uchimbaji wa madini hazitawahi kutokea, kampuni inaweza kupunguza athari zozote mbaya kwa kubuni mipango ya kudhibiti dharura na hali ya hatari. Kwa kuhusisha wanachama wa jamii husika katika kujaribu mipango hii ya kukabiliana na hali, kampuni zinaweza kusaidia kuhakikisha kuwa mipango inafanya kazi vizuri iwapo hali ya dharura ya kweli itatokea.

09 Malalamiko na Manung’uniko ya Jamii

Kampuni ambayo inaheshimu jamii za eneo husika hutaka kufahamu na kushughulikia masuala yao. Hii inajumuisha kubuni mchakato rasmi (unaoitwa mbinu ya kushughulikia manung’uniko ya jamii) ambao unawawezesha watu au makundi kutoka kwa jamii husika kuwasilisha malalamiko yao, ili masuala haya yasuluhishwe na kampuni. Kuna uwezekano kuwa wanajamii wataamini na kutumia mbinu hizi za kuwasilisha malalamiko iwapo kampuni itafichua jinsi ambavyo mbinu inatumika na hatua ambazo zinachukuliwa ili kuhakikisha kuwa malalamiko yanashughulikiwa kwa njia bora.

10 Usalama na Afya ya Wafanyakazi

Mazingira salama ni yale ambayo yanadumisha afya ya mwili na ya kiakili ya wafanyakazi. Mazingira safi ya kufanyia kazi kwa kawaida huwa yenye tija zaidi na maeneo ya kuchimba madini yenye hali nzuri za usalama yana fursa nzuri ya kuvutia wafanyakazi na wawekezaji. Kampuni ya kuchimba madini inaweza kuepuka na kupunguza hatari za usalama kwa kuwapa wafanyakazi wake vifaa vinavyofaa vya kujikinga na vyoo vinavyofaa na vifaa vya kuoshea mikono ambavyo ni salama kwa wanaume na wanawake. Kufuatilia ratiba za kazi kwa uwazi kunaweza pia kuzuia tabia za unyanyasaji zinazoweza kutokea.

11 Wafanyakazi wa Kike

Wafanyakazi wa kike wako katika hatari zaidi katika hali za kufanya kazi ambazo si salama na hazifai. Kampuni inaweza kuonyesha heshima yake kwa wafanyakazi wa kike kwa kuchukua hatua za kuzuia unyanyasaji na vurugu za kijinsia, pamoja na kuwapa wanawake nguo zinazofaa za kufanyia kazi na vifaa vya kujilinda. Mafunzo yanayofaa ni muhimu ili kuwasaidia wanawake na wanaume kuelewa jukumu la jinsia na kuboresha usawa wa kijinsia mahali pa kazi.

12 Majeraha na Vifo Vinavyotokea Mahali pa Kazi

Uchimbaji madini ni kazi hatari. Ajali hatari zaidi zinazotokea katika maeneo ya kuchimba madini bado zinaendelea kutokea duniani kote. Kampuni ya kuchimba madini inaweza kuepuka na kupunguza hatari za usalama wa mahali pa kazi kwa kufichua na kufanya uchunguzi wa ajali na vifo. Sekta ya uchimbaji wa madini inategemea zaidi wakandarasi, kwa hiyo ni muhimu kwa kampuni pia kutoa maelezo kuhusu vifo vyovyote vya watu wanaofanya kazi kwa wakandarasi, ili kutoa picha kamili zaidi ya hali ya usalama wa wafanyakazi wake.

13 Mafunzo ya Wafanyakazi

Kulingana na Shirika la Kimataifa la Wafanyakazi, hakuna mtu yeyote anayepaswa kuajiriwa ili kufanya kazi katika eneo la kuchimba madini isipokuwa mtu huyo awe amepokea mafunzo na maagizo yanayohitajika ya kumwezesha kufanya kazi kwa bidii na kwa usalama. Kwa hiyo, mafunzo hayapaswi tu kuzingatia afya na usalama na mbinu za kukabiliana na dharura, lakini pia ujuzi wa kiufundi. Hatua ya kuelimisha na kufunza wafanyakazi inaweza kusababisha kuwa na jopokazi lenye tija zaidi.

14 Mshahara wa Kuwezesha Kuishi Maisha Mazuri

Mshahara wa kuwezesha kuishi maisha mazuri ni ule ambao unawawezesha wafanyakazi na familia zao kumudu maisha ya msingi lakini ya kisasa, kuishi juu ya kiwango cha umaskini na kuweza kushiriki katika maisha ya kijamii na kitamaduni. Mshahara wa kuwezesha kuishi maisha mazuri ni haki ya msingi. Kampuni ya kuchimba madini ambayo huchukua hatua ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi wake na watu wanaofanya kazi kwa wakandarasi wanalipwa mshahara wa kuwezesha kuishi maisha mazuri inaweza kuimarisha uhusiano wake na wafanyakazi, kuboresha ari na tija ya wafanyakazi; na kuonyesha kuwa inaheshimu haki za wafanyakazi wake.

15 Malalamiko na Manung'uniko ya Wafanyakazi

Kampuni ambayo inaheshimu wafanyakazi wake hutaka kufahamu na kushughulikia masuala yao. Hii inajumuisha kubuni mchakato rasmi (unaoitwa mbinu ya kushughulikia manung'uniko ya wafanyakazi) ili kuwapa wafanyakazi njia ya kuwasilisha malalamiko ili masuala yao yanaweze kushughulikiwa na kampuni. Mbinu bora ya kushughulikia manung'uniko itasababisha kuwepo kwa mahusiano mazuri kati ya kampuni na jopokazi lake. Kampuni inaweza kuendeleza imani kwenye mchakato wa kushughulikia manung'uniko kwa kufichua jinsi mbinu ya kushughulikia manung'uniko inavyotumika na jinsi kampuni inavyochukua hatua ili kuhakikisha kuwa malalamiko yanashughulikiwa kwa njia bora.

Ili upate utaratibu kamili wa masuala yanayohusiana na uchimbaji madini wa kuwajibika, unaweza kutembelea tovuti ya Responsible Mining Foundation:
www.responsibleminingfoundation.org

Kwa maswali na usaidizi, tafadhali tuma barua kwa
contact@responsibleminingfoundation.org

Dokezo
Maudhui ya hati hii hayawakilishi maoni ya wafadhili, wadhamini na wafanyakazi wa Responsible Mining Foundation (RMF) na wengine walioshiriki katika mashauriano na waliohudumu kama washauri kwa hati hii.

Imechapishwa bila malipo kama bidhaa ya umma
Data na maudhui yote yaliyoandikwa yamepewa leseni chini ya Leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-NonCommercial 4.0 (CC BY-NC 4.0). Watumiaji wako huru kushiriki na kutumia nyenzo hii lakini ni lazima watoe shukrani kwa wahusika, watoe kiungo cha kuelekeza kwenye leseni na waonyeshe iwapo mabadiliko yalifanywa. Nyenzo iliyopewa leseni haipaswi kutumiwa kwa madhumuni ya kibiashara au kwa njia ya kubagua, kudhalilisha au kupotosha ukweli. Inapotajwa, ihusishe na: «Responsible Mining Foundation (RMF) (2020), '*Zana ya Kutathmini Eneo la Kuchimba Madini*'»